

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA**

Simu: +255 026 23222761-5
Fax No. +255 026 2322624
E-mail: cna@bunge.go.tz



Ofisi ya Bunge,
S.L.P. 941,
DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

Kamati za Kudumu za Bunge zitaanza kukutana Jumatatu tarehe 29 Agosti hadi tarehe 11 Septemba, 2022 Jijini Dodoma. Kamati hizo zinakutana kabla ya Mkutano wa Nane wa Bunge uliopangwa kuanza tarehe 13 Septemba, 2022.

Aidha, Kamati nne (4) zitaanza vikao tarehe 25 Agosti, 2022. Kamati hizo ni Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC), na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI.

Shughuli zilizopangwa kufanywa na Kamati katika vikao hivyo ni kama ifuatavyo:-

- a. Kamati ya Sheria Ndogo itafanya Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa wakati wa Mkutano wa Saba wa Bunge.
- b. Kamati Tisa (9) za Kisekta zitapokea na kujadili taarifa mbalimbali za utendaji.
- c. Kamati mbili (2) zinazosimamia matumizi ya fedha za umma zitachambua Taarifa ya Mdhambi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021.
- d. Kamati tatu zitafuatilia utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa za Mwaka za Kamati zilizowasilishwa Bungeni Mwezi Februari, 2022.
- e. Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) imepanga kupokea na kuchambua taarifa za uwekezaji wa mitaji ya umma ili kubaini iwapo uwekezaji huo una ufanisi na kuwa umezingatia taratibu na miongozo mujarabu ya biashara.
- f. Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama itapokea na kujadili Taarifa za Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki na za Wawakilishi wa Bunge la Tanzania katika Vyama vinne (4) vya Kibunge.

- g. Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti imepanga kupokea na kujadili Taarifa ya yatokanayo na Kikao kilichofanyika kwa mujibu wa Kanuni ya 124(1) ya Kanuni za Bunge kwa ajili ya majumuisho ya hoja zilizojitokeza wakati wa kujadili utekelezaji wa Bajeti za Wizara kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na Makadirio ya Matumizi ya Wizara hizo kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Vilevile itapokea taarifa zinazoiwezesha Kamati kufuatilia ukusanyaji na vyanzo vya mapato nchini.
- h. Kamati mbili (2) zitajadili miswada mitatu (3) ya sheria ikiwemo kupokea maoni ya wadau kuhusu miswada hiyo.

Ratiba za Shughuli za Kamati zote inapatikana katika Tovuti ya Bunge ambayo ni www.bunge.go.tz.

Imetolewa na:- Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa,
Ofisi ya Bunge,
S.L.P 941,
DODOMA.

22 Agosti, 2022.